BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Tano – Tarehe 15 Disemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Ripoti ya Sita ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa Mwaka 2021/2022.

**Waziri wa Afya:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Sita ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

124. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Zanzibar imebarikiwa kuwa na mandhari nzuri za fukwe mbali mbali ambapo kupitia fukwe hizo wananchi pamoja na wageni wetu huzitumia kwa ajili ya mazoezi na shughuli za kiutalii kama vile maeneo ya 'Zanzibar Beach Resort' na 'Zanzibar Ocean View'. Kwa kuwa baadhi ya maeneo hayo yana milima na miporomoko ya maji ambayo baadhi yake imekatika

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kuyafanyia matengenezo maeneo hayo.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

104. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Utumishi wa Umma ulio bora hautakiwi kufungamana na mirengo ya kisiasa. Hata hivyo, katika nchi yetu ya Zanzibar, ni kanuni inayofahamika kwamba Utumishi wa Umma ndio unaotekeleza ahadi za vyama vinavyopewa ridhaa na wananchi kuunda Serikali kupitia Ilani zao za Uchaguzi wa Zanzibar. Katika dhana ya Utawala Bora, utaratibu huo hautakiwi upunguze au uathiri misingi ya Utumishi wa Umma ya kutofungamana na mirengo ya siasa.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba kuna utekelezaji bora wa Ilani ya Chama, huku kukiheshimiwa Kanuni hiyo ya Utumishi wa Umma.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuwa na Sheria na Kanuni zinazoongoza utekelezaji wa ahadi za vyama vinavyopewa ridhaa na wananchi kuunda Serikali, kupitia Ilani zao za Uchaguzi wa Zanzibar.

105. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kinyume na matakwa ya Serikali, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (Zanzibar Anti-Corruption and Economic

Crimes Authority - ZAECA) haijaonyesha uwezo wa kuridhisha katika kufanya kazi yake ya msingi na muhimu ya kuzuia rushwa.

(a) Je, ni mpango upi endelevu wa Serikali wa kuiwezesha ZAECA kushiriki katika kutathmini utekelezaji wa mikataba mikubwa, matumizi ya rasilimali na fedha za umma kwa uhuru.

(b) Je, Serikali ina mpango gani endelevu wa kuiwezesha ZAECA kuwa na nyenzo, utaalamu na mfumo wa kufanya kazi zake za kuzuia na kupambana na rushwa kwa weledi na ufanisi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

2. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwanasua wananchi wake kiuchumi kwa kuwasogezea mikopo mbali mbali kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na njia nyengine mbali mbali, kumejitokeza tatizo kubwa la riba inayotakiwa kulipwa pamoja na marejesho ya mikopo hiyo.

Je, Benki yetu ya PBZ ina mpango na matarajio yepi ya kuwapunguzia riba wananchi wake hususan wenye kipato cha chini wanaokopa kupitia Benki hiyo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

31. MHESHIMIWA ABDULLA HUSSEIN KOMBO (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kiwanja cha Forodhani ni eneo mashuhuri Zanzibar linalotumiwa na watalii hasa kwa ajili ya kujipatia huduma za bidhaa za vyakula. Vile vile eneo hilo linawanufaisha vijana wengi kwa kuwapatia ajira kupitia shughuli mbali mbali wanazozifanya katika eneo hilo. Aidha, kwa upande wa mapato, Manispaa ya Mjini Zanzibar, inakusanya mapato mbali mbali ikiwa ni pamoja na sehemu za biashara zinazokodishwa kwa wafanyabiashara katika kiwanja hiki.

(a) Je, ni kiasi gani cha mapato kimekusanywa na Manispaa ya Mjini kutokana na kodi ya eneo hilo kwa kipindi cha

miaka miwili iliyopita.

(b) Je, Manispaa ya Mjini imetumia gharama za kiasi gani kwa ajili ya kuliimarisha eneo hilo, ili liweze kuvutia na kutumiwa zaidi na wafanyabishara na vijana, kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali.

(c) Je, ni Idara au Taasisi ipi inayotakiwa kukusanya mapato na kuliendesha eneo hilo.

41. MHESHIMIWA HABIB ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa waheshimiwa masheha wanafanya kazi ndani ya nyumba zao bila ya kuwa na ofisi maalum za kufanyia kazi hizo. Kwa kuwa hali hii inasababisha baadhi ya masheha wanapoondolewa katika nafasi zao, kushindwa kuwakabidhi nyaraka masheha wapya walioteuliwa.

Je, ni lini Serikali itawajengea masheha ofisi za kudumu ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri.

<u>**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**</u>

9. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Miongoni mwa kazi kubwa ya Serikali ni kuinua vipaji vya wasomi mbali mbali, ikiwa ni pamoja na wasomi wa fasihi na riwaya. Hata hivyo, katika jambo linalokosekana sana katika Serikali hasa za nchi zinazoendelea, ni kuwaenzi na kuwatunza wasanii wa fani za fasihi na riwaya.

(a) Je, kwa kiwango gani Serikali inawaenzi waandishi wetu wa fasihi na riwaya hapa nchini.

(b) Je, ni waandishi wangapi wa kazi za fasihi na riwaya, tamthilia na mashairi walioiletea heshima nchi yetu kupitia kazi zao.

(c) Je, Wizara inatumia utaratibu upi wa kuwaenzi na kuwawekea kumbukumbu nzuri waandishi hao kwa maslahi ya vizazi vijavyo.

10. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo :

Kwa kuwa lugha yetu ya Kiswahili imeendelea kukua na kufikia (kwa sasa) kuwa ni miongoni mwa lugha maarufu duniani inayozungumzwa na watu wasiopungua milioni mia mbili, na kwa kuwa Zanzibar ni sehemu kuu ama ni kitovu cha lugha hiyo, ikilinganishwa na sehemu nyengine yoyote Afrika ya Mashariki na duniani kote.

(a) Je, Kiswahili kinajikuza na kujieneza wenyewe au kinakuzwa na kuenezwa.

(b) Kama kinaenezwa, ni nani haswa anaewajibika kukikuza na kukieneza katika mataifa mbali mbali duniani.

(c) Je, kwa kiwango gani mwenye jukumu la kukikuza na kukieneza ametekeleza jukumu lake hilo na changamoto zipi zinazomkabili.

11. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Pamoja na majukumu yao mengi ya kuiwakilisha nchi yetu ya Tanzania, Mabalozi mbali mbali wanaoiwakilisha nchi yetu katika nchi rafiki, pia wana jukumu la kuikuza lugha yetu ya Kiswahili. Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwa kuwa Zanzibar ina nafasi kubwa ya kukieneza na kukiendeleza Kiswahili duniani kote, ikiwa ni pamoja na kupitia kwa Mabalozi wa Tanzania wanaoiwakilisha nchi yetu duniani kote.

Je, ni upi mchango wa Balozi zetu katika kukikuza na kukieneza pamoja na kutoa fursa mbali mbali za ajira kupitia lugha yetu ya Kiswahili.

57. MHESHIMIWA PANYA ALI ABDALLA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Zanzibar ina upungufu wa wataalamu wa utamaduni wenye sifa za kitaaluma zinazokubalika Kimataifa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasomesha vijana katika fani hii, ili kuwa na wataalamu wa kutosha.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

24. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa wananchi wa vijiji vya Shumba Vyamboni, Gombe, Bule na Mamoja wanategemea maji kutoka kisima kilichopo Shumba Vyamboni na kwamba kisima hiki hakina tenki (tangi) la kuhifadhia na kusambazia maji.

(a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwajengea tenki (tangi) wananchi hawa ili waweze kupata maji safi na salama kwa uhakika.

(b) Je, Wizara yako ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya maji katika vijiji hivi.

74. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tangi la Maji lililopo Kengeja Boshoki Shehia ya Kengeja ni bovu na halina uwezo wa kuhifadhi maji kwa sasa.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu suala hili.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kulifanyia matengenezo tangi hilo.

91. MHESHIMIWA SABIHA FILFIL THANI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tunaishukuru Serikali kwa kuwapatia wananchi wake maji safi na salama.

Je, ni lini Serikali itahakikisha huduma ya maji safi na salama itapatikana kwa wananchi wa Pongwe na Ndudu kwa matumizi yao na kuwavutia wawekezaji katika maeneo hayo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

27. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mbali ya upandaji wa nauli za usafiri wa anga, baharini na nchi kavu, bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa usafiri wa anga kwa upande wa kisiwa cha Pemba kutokana na kuongezeka kwa abiria na kupungua kwa ndege.

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea changamoto hii ambayo ni tatizo kubwa kwa usafiri wa ndege kisiwani Pemba.

(b) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kukabiliana na changamoto hii.

33. MHESHIMIWA ABDULLA HUSSEIN KOMBO (Jimbo la Mkoani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mwezi Machi mwaka 2019, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Zanzibar ilifanyiwa ukaguzi wa namna gani inatekeleza mikataba iliyoisaini ya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Baharini (International Maritime Organisation (IMO).

(a) Je, kupitia ukaguzi huo, Tanzania ilibainika kuwa na mapungufu mangapi na ya maeneo gani, Na kwa upande wa Zanzibar ukaguzi ulibaini mambo yepi.

(b) Ni mapungufu mangapi mpaka sasa yamesharekebishwa na kuwasilishwa utekelezaji wake.

(c) Ni athari gani nchi yetu ya Tanzania itapata ikiwa haitotekeleza mapungufu hayo na je Serikali imejipangaje kukabiliana na athari hizo.

134. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuboresha viwanja vyetu vya ndege Zanzibar, sambamba na kujenga Terminal 3 ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume. Kwa vile kuna teknolojia zinazohitaji ujuzi na utaalamu wa ufundi wa hali ya juu ambao umetumika na mitambo muhimu iliyopo hapo.

(a) Je, ni upi mpango wa Wizara utakaotumika katika kuwapatia mafunzo ya kiufundi, wafanyakazi wa mitambo hiyo ili kuepuka changamoto ambazo zinaweza kujitokeza baada ya kuondoka kwa wataalamu waliojenga jengo la Terminal 3 ya Uwanja wa Ndege huo.

(b) Kwa kuwa kuna upungufu wa wafanyakazi sambamba na wafanyakazi wa mkataba ambao wanafanya kazi zaidi ya miaka minane, Je, Wizara ina mkakati gani katika kutatua changamoto hii.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

14. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika juhudi kubwa inayofanywa na Serikali yetu hasa hii ya awamu ya nane, ni kulitilia nguvu za ziada suala zima la ujasiriamali, ili wanafunzi wetu wanaomaliza elimu zao waweze kujitegemea na sio kulazimisha kuajiriwa Serikalini.

(a) Kwa kuwa Wizara yako ndio yenye dhamana ya kuwaandaa wanafunzi katika elimu ya vitendo, je, kwa kiasi gani mitaala ya elimu inawasaidia wanafunzi kuwa wajasiriamali wazuri.

(b) Je, kwa kiasi gani na kuanzia ngazi ipi ya elimu, suala la elimu ya ujasiriamali limepewa mazingatio katika maboresho ya mitaala yetu ya elimu.

20. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kufaulu kwa wanafunzi huambatana sana na namna wanavyoweza kutumia vifaa bora vya kisasa vya kufundishia wanafunzi hao.

Je, kwa kiwango gani Wizara yako ina matarajio ya kugawa vifaa kama vile televisheni na ‘projectors’ katika skuli za Mwanakwerekwe, japo awamu kwa awamu, ili kukuza uelewa wa wanafunzi na kuondokana na ufundishaji wa kimazoea.

128. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Miaka ya 1980 na 1990, Serikali kupitia Wizara ya Elimu ilikuwa na utaratibu wa kuezeka majengo ya mabanda ya skuli ambayo wananchi wameyajenga kwa njia ya kujitolea.

Je, hivi sasa Serikali ina mpango gani juu ya uezekaji na kuyapiga plasta majengo hayo, ili watoto wetu wapate kuyatumia kwa kusomea.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

47. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Tunaipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi kubwa inazozichukuwa katika kuwaletea wananchi wake maendeleo kupitia miradi mbali mbali yenye tija kwa nchi yao ya Zanzibar. Pamoja na juhudi hizo, wananchi wetu wamekuwa wakisikitishwa na kugongana kimaono na kitaalamu kwa wataalamu hao wakati wote ni watumishi wa Serikali moja. Hali kama hii inashuhudiwa katika Mji Mkongwe wa Zanzibar katika ujenzi wake na kuhifadhiwa kwake.

Je, kwa kiasi gani wataalamu wa akilojia wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale wanashirikishwa katika kufanya 'Heritage Assessment Survey' kabla na wakati wa harakati za uchimbaji na ujenzi unaofanyika katika Manispaa yote ya Mji Mkongwe Zanzibar.

48. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Falsafa ya Uchumi wa Buluu ina mafungamano makubwa na utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

Je, Idara hii inaitekelezaje falsafa ya dhana ya Uchumi wa Buluu katika kuchangia pato la Taifa.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

129. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali iliyopo madarakani ya Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi imeanzisha Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kwa hatua ya mwanzo imewapatia wavuvi maboti. Tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Nane, lakini kuna tatizo la uharibifu wa kuyang'oa matumbawe hasa kwa watu wanaojihusisha na uvuvi wa juya (nyavu ndogo).

(a) Je, wavuvi wa juya watachukuliwa hatua gani za kisheria kwa uharibifu wa matumbawe.

(b) Je, ni adhabu gani hutolewa kwa wanaopatikana na kosa hilo.

**Wizara ya Afya:**

86. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuna baadhi ya wafanyakazi wa taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hawapatiwi huduma ya bima ya afya ambayo ingewasaidia kupunguza makali ya gharama za maisha hasa upande wa sekta ya afya.

Je, Serikali ina mpango gani utakaohakikisha wafanyakazi wote waliochini ya Serikali wanapatiwa huduma hii.

94. MHESHIMIWA SABIHA FILFIL THANI (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Naishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga hospitali za Wilaya kupitia fedha za UVIKO 19.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za madaktari karibu na hospitali hizo ili ziweze kutoa huduma kwa ufanisi.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

3. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

   Kwa muda mrefu sasa Serikali yetu imekuwa ikitegemea kibiashara mazao ya karafuu na mwani, ambayo kwa kweli tunakubali kuwa yamekuwa na tija kubwa kwa Taifa letu.

   Ukitoa mazao hayo ya karafuu na mwani, Je, Serikali inatoa kipaumbele cha mazao yepi mengine kibiashara, ili wananchi na wakulima wetu wajikite zaidi kuyalima kwa lengo la kuinua hali zao za kimaisha.

67. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

   Je, katika msimu huu wa uchumaji wa karafuu wa mwaka 2022 mpaka hivi sasa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) limeshanunua tani ngapi za karafuu na tani ngapi limesafirisha nchi za nje.

123. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

   Kwa kuwa wakati wa uchumaji wa zao la karafuu, wapo wananchi kwa bahati mbaya hupatwa na mitihani ya kuanguka mikarafuu, huku Serikali yetu ikiwa inafahamu umuhimu wa kuwapatia angalau fidia kwa ajili ya kujisaidia kutokana na ajali hizo.

   (a) Je, urataribu wa kupatikana fidia hiyo kwa walengwa hao ukoje.

   (b) Katika kupatikana kwa fidia hiyo, je kuna hitajio la umri maalumu kwa waliopatwa na ajali hiyo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

82. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kuna uvamizi wa kiwanja cha Maendeleo ya Jamii, Shehia ya Chukwani upande wa Buyu.

(a) Je, Serikali inalifahamu suala hilo.

(b) Je, kuna mkakati gani wa kutatua changamoto hiyo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Ripoti ya Sita ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa Mwaka 2021/2022.

**Waziri wa Afya:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

**Zanzibar,**
**15 Disemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**